


Ruthu Ni Rafiki Mshikamanifu

RUTHU SURA YA 1-4

NAOMI, MJANE KUTOKA MOABU, ALIAMUA KURUDI KATIKA NCHI YAKE, ISRAELI. BINTI-WAKWE ZAKE WAWILI, **RUTHU** NA **ORPA**, WALIANZA SAFARI PAMOJA NAYE.



BAADA YA KUTEMBEA KWA MUDA FULANI, NAOMI AKASIMAMA NA KUWAAMBIA RUTHU NA ORPA.




BINTI ZANGU, WAUME WENU WAMEKUFA, NA MNAPASWA KUTAFUTA WAUME WAPYA KATIKA **NCHI YENU, MOABU**.
RUDINI KILA MMOJA NYUMBANI KWA MAMA YAKE.





MIMI
SITAKI
KUONDOKA, LAKINI
RUTHU, NAOMI
ANASEMA KWELI.




MOABU NDIYO
MAHALI PEKEE AMBAPO
TUMEISHI! **MAMA** ZETU
WAKO MOABU, **FAMILIA** ZETU
ZIKO MOABU, MARAFIKI WETU
WAKO MOABU.

MIMI
NINARUDI
NYUMBANI.

LAKINI ORPA,
NAOMI NI FAMILIA YETU
PIA. NA YEHOVA,
MUNGU WAKE, NI
MWENYE
REHEMA NA FADHILI.
MIUNGU YA MOABU NI
MIKATILI.

TAZAMA! **ORPA**
ANARUDI KWA WATU
WAKE NA MIUNGU YAKE.
RUDI PAMOJA
NAYE.



HAPANA...
MIMI
SITAKUACHA.

UENDAKO
WEWE
MIMI
NITAENDA.

WATU WAKO
WATAKUWA
WATU
WANGU.

NA
MUNGU WAKO
ATAKUWA
MUNGU
WANGU.

WALIPORUDI ISRAELI, RUTHU ALIKUSANYA CHAKULA KWA AJILI YAKE NA NAOMI KWA KUOKOTA MASALIO YA SHAYIRI KATIKA SHAMBA LA MWANAMUME ALIYEITWA BOAZI.

HUYU MWANAMKE KIJANA NI NANI?

ALIRUDI PAMOJA NA NAOMI KUTOKA MOABU. HAJAKETI TANGU ASUBUHI.

YEHOVA NA AKUBARIKI, RUTHU. KILA MTU JIJINI ANAJUA KWAMBA WEWE NI MWANAMKE BORA SANA.

BOAZI ALIMWOA RUTHU, NA WAKAPATA MWANA ANAYEITWA OBEDI. MJUKUU WA OBEDI ALIKUJA KUWA MFALME ANAYEJULIKANA SANA WA ISRAELI. JE, UNAJUA NI MFALME YUPI? (SOMA RUTHU 4:22.)

TUNAJIFUNZA NINI KUTOKANA NA HADITHI HII?

RUTHU ALIONYESHAJE UPENDO MSHIKAMANIFU KUMWELEKEA NAOMI?
DOKEZO: RUTHU 1:14, 16, 17; 2:11, 12.

YEHOVA ALIONYESHAJE UPENDO MSHIKAMANIFU KUMWELEKEA RUTHU NA NAOMI?

DOKEZO: RUTHU 4:13-15.

WEWE UNAWEZAJE KUONYESHA UPENDO MSHIKAMANIFU KUELEKEA RAFIKI ZAKO?

DOKEZO: METHALI 17:17; 18:24.